

MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA MPIMBWE ANAWATANGAZIA WANANCHI WOTE KUWA:

HALMASHAURI INAKUSUDIA KUWASHIRIKISHA WAFANYABIASHARA KUWEKA UZIO WAKUDUMU KWA KUJENGA MADUKA YA BIASHARA KUZUNGUKA ENEO LA CHANZO CHA MAJI MAJIMOTO.

MADHUMUNI YA MABORESHO YA UZIO WA CHANZO CHA MAJI YA MOTO:

- I) KUSUDIO HILI LINALENGA KULINDA CHANZO KWA KUZUIA UHARIBIFU WA MAZINGIRA, KUTUPA TAKA, KUCHOMA MOTO, KUJISAIDIA NA KURINGIZA MIFUGO.
- II) KUSUDIO HILI LINALENGA KUENDELEZA ENEO HILI NA KUWEKEA VIVUTIO MBALI MBALI UPANDE WA NDANI KUFANYA ENEO LIWE LA UTALII.

JINSI YA KUBORESHA:


MKURUGENZI ANA WAKARIBISHA WADAU (WANANCHI) WENYE KUHITAJI KUJENGE MADUKA KUZUNGUKA ENEO LA CHANZO CHA MAJI KWA KUZINGATIA RAMANI NA MICHORO ILIYOPO WALETE MAOMBI.

JINSI YA KUJENGA

1. WADAU WOTE WANAO HITAJI WATAJAZA FOMU YA MAOMBI YA KUPATIWA ENEO LA KUJENGA KIBANDA.
2. FOMU NI TSHS. 10,000.00 INAPATIKANA KWA MHANDISI WA UJENZI, FOMU INA MAELEKEZO YOTE MUHIMU.
3. GHARAMA ZA UJENZI NA RAMANI YA KIBANDA UTAPEWA NA MHANDISI BAADA YA KUCHAGUA AINA YA BIASHARA UNAYO KUSUDIA KUIFANYA (VIBANDA VIPO KWA MPANGILIO WA AINA YA BIASHARA).
3. BAADA YA KUJENGA KIBANDA, UTAKIMILIKI KWA KULIPA NUSU YA KODI YA PANGO HADI GHARAMA ZA UJENZI ULIZO TUMIA ZIMALIZIKE NDIPO UTALIPA KODI YOTE YA PANGO KAMA MPANGAJI WA HALMASHAURI.

FAIDA ZA UJENZI HUU WA VIBANDA KWA MJI WA MAJIMOTO:

1. YATAKUWA MADUKA MAKUBWA YENYE NAFASI YA KUFANYA BIASHARA
2. MADUKA YATAPENDEZESHA MJI KWA JINSI YALIVYO ANDALIWA KITAALAM
3. NI FURSA KWA WAFANYA BIASHARA WENGI ZAIDI KUPATA ENEO LA BIASHARA MJINI/MAJIMOTO
4. NI UZIO WA ENEO LA CHANZO CHA MAJI WENYE MANUFAA.

  
MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA (W) MPIMBWE